# STANDARD SIX MID TERM ONE EXAM 2018

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

---

**Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza pengo.**

Maji ni muhimu sana ___1___ maisha ya binadamu. Miili ___2___ huhitaji ___3___ maji ya kutosha ili kuondoa uchafu ulio ndani. Isitoshe, wakati wa ___4___, yaani ukosefu wa mvua, mimea ___5___ maji ili iendelee kunawiri. Ukweli ni kwamba nchi ___6___ ambazo hazina maji ya kutosha ___7___ sana kiuchumi. Meli na vyombo ___8___ pia husafiria kwenye maji. Hatufai kuyamwaga maji ___9___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kwa | B. katika | C. ndani ya | D. juu ya |
| 2. | A. wetu | B. zetu | C. mwetu | D. yetu |
| 3. | A. tuyanywe | B. tukunywe | C. tuinywe | D. tunywewe |
| 4. | A. ukame | B. masika | C. kipupwe | D. upepo |
| 5. | A. hunywa | B. huwekwa | C. hunyunyiziwa | D. hupewa |
| 6. | A. mingi | B. nyingi | C. zingine | D. mengi |
| 7. | A. hunufaika | B. hujengeka | C. husaidika | D. huathirika |
| 8. | A. vingine | B. vyote | C. zote | D. nyingine |
| 9. | A. machafu | B. ile | C. ovyoovyo | D. vizuri |

Mvua kubwa ___10___ sana usiku ___11___. Tulipokuwa tukielekea ___12___ asubuhi, tulitelezateleza nusura tuanguke. Tulivisikia viatu vyetu vikiwa ___13___ sana. Tuliamua kutembea ___14___ kwa sababu tulielewa kuwa mwenda pole ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. ulinyesha | B. ilinyesha | C. yalinyesha | D. kulinyesha |
| 11. | A. hiyo | B. hilo | C. huyo | D. huo |
| 12. | A. shuleni | B. kwa shule | C. shule | D. kwenye shuleni |
| 13. | A. mzito | B. nzito | C. vizito | D. mazito |
| 14. | A. upole | B. kwa upole | C. polepole | D. haraka |
| 15. | A. hufika | B. hajikwai | C. hujikwaa | D. haanguki |

**Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.**

**16.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo;
Darasa letu lina dirisha kubwa.
A. Madarasa zetu zina dirisha kubwa.
B. Darasa zetu zina madirisha makubwa.
C. Darasa letu lina madirisha makubwa.
D. Madarasa yetu yana madirisha makubwa.

**17.** Saa 8.45 kwa maneno ni:-
A. saa tisa na robo
B. saa tisa kasorobo
C. saa tatu kasorobo
D. saa mbili kasorobo.

**18.** Tunasema *ringa* kama *tausi* lakini bahati kama:-
A. ya mtende
B. mchana
C. malika
D. sungura.

**19.** Maneno kama **kuja** na **kucha** huitwaje?
A. Visawe
B. Vitate
C. Vitawe
D. Vitenzi

**20.** Maneno yafuatayo yanapatikana katika ngeli gani? Kipepeo, kiwete, kiwavi.
A. Ki-vi
B. A-wa
C. U- I
D. Li-ya

**21.** Tegua kitendawili :
Popo mbili zavuka mto.
A. Magurudumu
B. Macho
C. Kamasi
D. Garimoshi

**22.** Msemo upi una maana ya kuvumilia bila kulalamika?
A. Tia juhudi.
B. Kata tamaa.
C. Kula mwata.
D. Kufa kikondoo.

**23.** Kanusha: Yeye amekula sima.
A. Yeye hajala sima.
B. Yeye hali sima.
C. Yeye hajakula sima.
D. Yeye hatakula sima.

**24.** Andika katika hali ya kutendewa:
Mti umeangukia nyumba.
A. Mti umeangusha nyumba.
B. Mti umeangushwa na nyumba.
C. Nyumba imeangukiwa na mti.
D. Nyumba imeangushwa na mti.

**25.** Kielezi ni kipi katika sentensi ifuatayo?
Mtoto yule anacheza mpira vizuri.
A. vizuri
B. mpira
C. yule
D. anacheza

**26.** Sehemu ya nyuma ya kichwa huitwaje?
A. Nyonga
B. Kisogo
C. Kisugudi
D. Paji

**27.** Andika katika hali ya udogo.
Njia hiyo ina watu wengi.
A. Kijia hilo lina watu wengi.
B. Kijia hicho kina watu wengi.
C. Jia hilo lina majitu mengi.
D. Kijia hicho kina vijitu vingi.

**28.** Ndugu wa mke wangu nitamwitaje?
A. Mwamu
B. Mpwa
C. Wifi
D. Binamu

**29.** Ukigawa chungwa kwa watoto watatu, kila mmoja atapata:-
A. robo
B. sudusi
C. thuluthi
D. thumni.

**30.** Chagua methali inayomaanisha kuwa mtu hafai kumdharau ndugu na kumthamini rafiki.
A. Damu ni nzito kuliko maji.
B. Bendera hufuata upepo.
C. Bandu bandu huisha gogo.
D. Jina jema hung'aa gizani

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31-40.**

Iwapo matukio ya hivi karibuni ni mizani kamili ya kutathminia maoni na matamanio makuu ya Wakenya, basi wabunge wetu hawana budi kuzinduka kutoka kwenye lepe la usingizi na kuwajibika kenyekenye. Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo. Wakenya kwa umoja sasa wanataka wawakilishi wao kuwajibika barabara kitaifa kwa masuala nyeti ya ulipaji ushuru, kuunganisha nchi, kutoa mwongozo maridhawa pamoja na kuhakikisha kwamba watu wanapata huduma muhimu.

Wananchi wanataka bunge ambalo linatii sheria; sheria ambazo wanaozibuni, kutunga na kuzipitisha ni wao. Kwa nini mpaka sasa hata baada ya miaka zaidi ya hamsini tuwe tunazungumzia suala la uhuru wa kutangamana, kuishi popote ama kuwa na mali popote nchini? Viongozi hawastahili kutumia ukabila kila mara ili kuchaguliwa ama kujipatia nafasi mbalimbali za kitaifa.

Tunatumai kuwa watajifunza kutokana na rais mstaafu wa Marekani na ambaye ana mizizi yake hapa nchini; Barack Obama. Je, aliwezaje kuchaguliwa? Ni rahisi; sera. Una sera gani za kitaifa? Ubinafsi, unafiki na ufisadi miongoni mwa viongozi wetu wa kisiasa ni tabia ambayo hawana budi kuivua na kufua ili Kenya itakate kiutawala. Ni kwa vipi viongozi watataka raia walipe ushuru na kodi ilhali wao wafanye kilinge na kudai hawastahili kutozwa ushuru? Tunahitaji kuongoza kwa vitendo.

Inasikitisha maana wao ndio wanaosema ni nani ama wapi ushuru huo utatumika. Je, haihalisi basi kwamba wanastahili kulipa kwanza? Mshahara wa mbunge ni mkubwa sana kuliko wa watu wangapi nchini? Marupurupu nayo? Ni vyema iwapo wabunge wetu watajiondolea haya kwa kuwa kielelezo kwa taifa hili.

Kwa hali na mali, wananchi wanastahili kuungana na mashirika yanayotetea haki za binadamu na wadau wengine kuwatia shime ili wasipinde wajibu huu muhimu wa kitaifa na kuhakikisha kuwa haki inatendwa.

31. Kulingana na matukio ya hivi karibuni:-
   A. wakenya wamefurahishwa na wabunge
   B. wakenya hawaridhishwi na wabunge
   C. Kenya haihitaji watu bungeni
   D. wabunge wetu ni waadilifu.

32. Wanachohitaji wakenya kutoka kwa wabunge kulingana na makala haya ni:-
   A. uwajibikaji  B. pesa
   C. siasa  D. barabara.

33. Ni jambo gani ambalo wabunge hawataki kufanya kulingana na kifungu?
   A. Kuwatenganisha wananchi.
   B. Kushiriki vikao bungeni.
   C. Kupitisha sheria za nchi.
   D. kulipa ushuru.

34. Kazi ya wabunge ni gani?
   A. Kupitisha sheria walizotungiwa.
   B. Kuwatenganisha wananchi kikabila.
   C. Kubuni, kutunga na kupitisha sheria.
   D. Kuchunguza na kubadili sheria zote.

35. Imepita miaka mingapi tangu tulipojipatia Uhuru?
   A. Nusu karne  B. Elfu mbili
   C. Mia moja  D. Hatujaambiwa

36. Haki za Mkenya si pamoja na:-
   A. kumiliki mali popote nchini
   B. kuepuka ulipaji wa ushuru
   C. kutangamana na watu wengine
   D. kuwachagua viongozi anaowataka.

37. Viongozi huwachochea watu kwa:-
   A. kuanzisha shughuli za maendeleo
   B. kupiga siasa kutafuta kura
   C. kuwaajiri wananchi kazi mbalimbali
   D. kueneza ukabila nchini.

38. Barack Obama:-
   A. ni rais wa Marekani
   B. alikuwa rais wa kwanza Marekani
   C. alikuwa rais wa Marekani
   D. alikuwa rais wa Kenya.

39. Ili kiongozi aweze kuchaguliwa, ni muhimu:-
   A. awahonge wapiga kura
   B. awe mzee anayeheshimika
   C. awe na mali ya kutosha
   D. awe na sera nzuri.

40. Mashirika ya kutetea haki za binadamu huhakikisha kuwa:-
   A. wananchi hawadhalilishwi
   B. wabunge wanatozwa ushuru
   C. viongozi wabaya hawachaguliwi
   D. marupurupu ya wabunge yamepunguzwa.

***Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia 41 mpaka 50.***

Hapo zamani za kale, paliondokea mwanamume mmoja shujaa, katika jamii ya Wakamba. Shujaa huyo aliitwa Masaku. Alichangia sana jamii ya Wakamba kwa mambo mengi ambayo yaliwafungua macho wakabaini umuhimu wao.

Masaku alikuwa mtabiri. Alitabiri kuletwa kwa mambo yaliyohusiana na majani ya miti. Utabiri huu ulimaanisha kuwa wakoloni wangeleta pesa katika jamii hii. Mambo hayo yalifanyika alivyotabiri. Walioamini na kusadiki utabiri huu walifaidika pakubwa na wakoloni walipofika katika nchi yao.

Jina la mji wa Machakos lilitokana na shujaa huyu. Hata sasa, wakamba huuita mji huu 'Masaku'. Wakoloni walipofika katika ardhi ya wakamba walishindwa kutamka jina Masaku, hivyo wakafisidi jina hili na kuwa 'Machakos' kama linavyotumika katika maandishi.

Masaku alikuwa daktari wa mitishamba. Aliweza kuwatibu watu wa jamii yake walipougua. Dawa zake ziliaminika na kutambulika mno ndani na nje ya Ukambani. Aidha, aliaminika na kujulikana kwa kuwatibu wanyama. Maarifa haya ya kuwatibu wanyama yalifanya mifugo kuongezeka katika jamii yake. Vilevile, Masaku anatambuliwa kuwa shujaa aliyewaongoza Wakamba kuwa wafanyabiashara. Aliweza kuwa na ushirikiano na Wakoloni ambao walikuwa wanunuzi wa bidhaa kutoka jamii yake. Wakamba watajika kama vile Chifu Kivoi, kupitia biashara waliweza kuleta bidhaa za kigeni katika jamii hii.

Masaku alikuwa mpiganaji hodari. Aliongoza vita dhidi ya jamii nyingine. Yeye alishiriki kuilinda jamii ya wakamba kwa uaminifu mno. Aliilinda jamii yake kutokana na jamii zilizoteka mifugo yao. Jambo hili lilichangia sana ustawi wa jamii ya wakamba.

Masaku aliiongoza jamii yake kutafuta ardhi yenye rutuba. Aliweza kuwasaidia kujipatia ardhi katika milima, kwa mfano Mlima Mbooni. Wao walianza upanzi wa mimea katika milima hii iliyokuwa bora.

Jamii ya wakamba ilimpoteza shujaa Masaku alipouawa katika vita kati ya wakamba na wamaasai. Bila shaka, yeye alikuwa shujaa katika mambo mbalimbali maishani.

**41.** Masaku alikuwa:-
A. mkoloni shujaa wa Ukambani
B. shujaa aliyepigana dhidi ya wakamba
C. mtabiri shujaa aliyewatetea wakamba
D. mfanya biashara maarufu.

**42.** Miongoni mwa mambo aliyotabiri masaku yakatokea kuwa kweli kulingana na kifungu ni:-
A. kuja kwa wakoloni na garimoshi
B. kuletwa kwa pesa na wakoloni
C. kuwepo kwa majani ya miti
D. kuondoka kwa wakoloni nchini.

**43.** Walioamini na kusadiki utabiri wa Masaku:-
A. walifaidika B. walijuta
C. waliangamia D. waliaibika.

**44.** Mji wa masaku ulipewa jina Machakos na:-
A. Masaku B. wenyeji
C. wazee D. wakoloni.

**45.** Waliofaidika na matibabu ya Masaku ni:-
A. wakamba pekee
B. wakamba na wakoloni
C. watu na mifugo
D. watu na mitishamba.

**46.** Mifugo ya wakamba iliongezeka kwa sababu ya:-
A. utabiri wa Masaku
B. kutibiwa na Masaku
C. kufugwa na Masaku
D. kutibiwa na wakoloni.

**47.** Chifu Kivoi ametajwa kama:-
A. kiongozi maarufu wa wakamba
B. mtabiri maarufu wa mambo
C. mfanya biashara maarufu
D. mgeni aliyeuza bidhaa Ukambani.

**48.** Masaku alikuwa mpiganaji hodari kwa kuwa:-
A. aliongoza vita dhidi ya wakoloni
B. alikabiliana vilivyo na maadui wa wakamba
C. aliwaongoza wakamba kushiriki biashara
D. alishirikiana na wakoloni kuleta maendeleo.

**49.** Ardhi yenye rutuba ilihitajika ili:-
A. kuweka mifugo
B. kushiriki zaraa
C. kuepuka mashambulizi
D. kuendeleza biashara.

**50.** Hatimaye, Masaku aliuawa na:-
A. wakoloni B. maradhi
C. uzee D. wamaasai.